

MAELEZO YA KAZI ZA MTOA HUDUMA WA KUJITOLEA KUTOKA ASASI YA KIRAIA (AZAKI)

JUKUMU LA MSINGI:

Kuwezesha majadiliano kuhusu mabadiliko ya tabia kwa ajili ya vikundi vya kusaidiana, kuwaunganisha wanajamii kwenye huduma. Kuhamasisha masuala ya lishe kwa kutumia majukwaa mbalimbali kama vile mikutano ya TASAF, maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji n.k

MAIN DUTIES:

1. Kutambua vikundi vya kusaidiana ambavyo vinapenda kujifunza na kuhamasisha lishe bora, usafi na usalama wa maji, chakula na mazingira, malezi na makuzi ya awali, na kilimo. Hutembelea vikundi, vyama vya kuweka na kukopa, mikutano ya TASAF, Vikundi vya dini msikitini na makanisani, Vikundi vya kusaidiana kimaendeleo/ uchumi, vikundi vingine vya wanaume na wanawake, kamati za maendeleo ya kata n.k.
2. Hubainisha ni vikundi gani vya jamii vinaonesha dhamira kwa kuboresha masuala ya afya. Weka kipaumbele kwa vikundi vinavyotaka kuboresha afya na viwe na wanakikundi ambao wanaweza kushawishi tabia/ matendo chanya kuhusu lishe, usafi na usalama wa maji, chakula na mazingira, malezi na makuzi ya awali, na kilimo – kama vile vyenye kina baba, bibi, na mama.
3. Hufanya ushawishi kupata nafasi kwenye mikutano ili:
 - a. Kujadili umuhimu wa lishe bora kwa watoto
 - b. Zungumza kuhusu matendo/tabia mahususi ambazo watu wanaweza kuiga ili kuboresha afya na maendeleo ya watoto
 - c. Bainisha mambo/vitu ambavyo wanakikundi wanaweza kifanya kuboresha ukuaji na maendeleo ya watoto
 - d. Wahamasisha wanakikundi ili wajenge dhamira na kufanya matendo mahususi ili kuboresha afya
 - e. Wahamasisha wanakikundi wajenge dhamira na kuongea na wanajamii wengine kuhusu walichoifunza
4. Hufufua vikundi vya kusaidiana vilivyopo ambavyo huwalenga akina mama walio ndani ya kipindi cha siku 1000 (yaani wenye ujauzito au wenye watoto chini ya umri wa miaka miwili) na watu wenye ushawishi kwao, wakiwemo akina baba na bibi. Kama hakuna uwezekano au tija kwa kufufua vikundi vilivyopo, huanzisha vipya.
5. Hukusanya takwimu/taarifa kutokana na matembeleo ya vikundi vya kusaidiana. Hurejesha fomu zilizojazwa kwa mfanyakazi wa ufuatiliaji na tathimini wa AZAKI .
6. Fanya uratibu na AZAKI mara kwa mara.

